# MwanaHisa

CRDB BANK PLC Toleo la Julai, 2017


## YALIYOMO


Maazimio ya Mkutano Mkuu wa 22 ........................1

Mwanahisa Wetu: Mzee Mbonde..................2&3

Malipo ya gawio kwa mwaka 2016.................4

Je Wajua taratibu za kudai gawio? ............. 4&5

Jinsi ya Kurithisha Hisa zako ........................5&6

Matukio Katika Picha ...........7

Kibonzo: ............................8


## ANUANI


Mhariri Mwanahisa
CRDB Bank Plc
Office Accomodation Scheme
Mtaa wa Azikiwe, Ghorofa ya 4
S. L. P. 268 Dar es Salaam

Simu Na: 002 - 21174421-002, - 2114237
Fax No: 002-2131005
investorrelations@crdbbank.com
Tovuti: www.crdbbank.com


### MAONI KUTOKA KWA MWANAHISA

Wanahisa wanapewa fursa ya kufikisha maoni, ujumbe au mapendekezo katika jarida hili kwa kutumia a nuani inayoonekana hapo juu.

## Maazimio ya Mkutano Mkuu wa 22

Tarehe 20 Mei, 2017 mji wa Arusha ulishuhudia Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa wa Benki ya CRDB uliofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa (AICC) jijini Arusha. Ulikuwa ni Mkutano wa 22 na kama ilivyo desturi, ulifana kwani wanahisa walipitisha maazimio na maamuzi muhimu kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya Benki yao.



*Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya CRDB Bw. Ally Laay akiwasilisha taarifa wakati wa Mkutano Mkuu wa 22 wa wanahisa uliofanyika katika ukumbi wa kituo cha Kimataifa cha Mikutano (AICC) jijini Arusha Tarehe 20, Mei 2017*

Mkutano Mkuu wa Wanahisa hufanyika kila mwaka kama inavyoelekezwa katika Katiba ya Benki na kwa mujibu wa matakwa ya vigezo vya Utawala Bora. Mkutano Mkuu ulitanguliwa na Semina ya Wanahisa iliyofanyika tarehe 19 Mei 2017 katika ukumbi huo huo na kufuatiwa na hafla fupi iliyofanyika katika Hoteli ya Mount Meru. Hafla hii ilifana sana kwani wanahisa walipata burudani, chakula, vinywaji na kupata fursa ya kuwasiliana kwa karibu na menejimenti na wakurugenzi wa Benki.

Semina ya Wanahisa ilitoa fursa ya pekee kwa washiriki kujifunza kupitia mada nne (4) zilizowasilishwa. Mada zilikuwa: Fursa na Changamoto za Uwekezaji kwenye Hisa, Taratibu mbalimbali ambazo Mwanahisa anapaswa kuzifahamu, Mambo yanayotanabaisha thamani na bei ya Hisa na Utawala Bora katika kukuza thamani ya uwekezaji.



CRDB BANK
The bank that listens

Mkutano ulihudhuriwa na wanahisa zaidi ya 1,000 kutoka mikoa na maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi, waliowakilisha zaidi ya asilimia 70 ya hisa za Benki. Wanahisa walishiriki kikamilifu katika mijadala kuhusu dondoo mbalimbali zilizowasilishwa na hatimaye kutoa maoni na kuuliza maswali ambayo yatasaidia bodi na menejimenti kuboresha uendeshaji wa shughuli za Benki.
Taarifa ya kustaafu kwa wakurugenzi watatu (3) wa bodi ilipokelewa. Wakurugenzi hao ni Mheshimiwa Frederick T. Sumaye, Bw. Bede P. Lyimo na Bw. Kai Kristoffersen.

**Wajumbe wa Mkutano Mkuu waliidhinisha Maazimio yafuatayo:**

- Gawio la shilingi 10 kwa kila hisa kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Desemba 2016
- Ada ya Wakurugenzi kwa mwaka 2017 ya shilingi 751,928,576
- Dkt. Neema Mori Munisi alichaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Bodi kutoka kundi la wanahisa wenye hisa chini ya asilimia moja
- Kampuni ya PricewaterhouseCoopers iwe Mkaguzi wa Hesabu wa Kampuni za CRDB kwa mwaka 2017
- Mkutano Mkuu wa 23 wa Wanahisa ufanyike jijini Arusha tarehe 19 Mei, 2018 katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa (AICC) kwenye Ukumbi wa Simba
- Sala ya Mkutano Mkuu.

# Mwanahisa Wetu - Mzee Mbonde

***Katika makala hii tunakuletea mazungumzo yaliyofanyika na mmoja wa wanahisa waanzilishi wa Benki akizungumzia faida za mwanahisa kuhudhuria Mkutano Mkuu na Semina.***

Huwezi kuzungumzia watangazaji maarufu wa redio nchini Tanzania bila kutaja jina la Salim Mbonde, ambaye amekuwa kwenye fani ya utangazaji kwa zaidi ya miaka 30. Mzee Mbonde alikuwa mtangazaji nguli wa Shirika la Utangazaji la Taifa (zamani ikiitwa Radio Tanzania Dar es Salaam) kabla ya kustaafu hivi karibuni. Mzee Mbonde ni mmoja wa wanahisa wa Benki ya CRDB waliohudhuria Mkutano Mkuu wa Mwaka uliofanyika Arusha tarehe 20, Mei 2017. Pia alihudhuria Semina ya Wanahisa iliyofanyika siku moja kabla ya Mkutano Mkuu.

"Moja ya mambo muhimu niliyojifunza wakati wa Mkutano Mkuu na Semina mwaka huu ni umuhimu wa wanahisa kusoma kwa makini na kuelewa taarifa zinazotolewa kwao na pale inapobidi kupata ufafanuzi wa masuala mbalimbali kutoka matawini au uongozi wa juu wa Benki, alisema Mzee Mbonde."

Alisema ni muhimu kwa wanahisa kuhudhuria mikutano na semina zinazofanyika kila mwaka ili kuweza kujua mambo mbalimbali yanayowahusu. "Mikutano na semina inatufundisha na kutukumbusha wajibu wetu kama wawekezaji na pia majukumu ya menejimenti na Bodi kwa wanahisa. Vilevile, ni nafasi ya kujua fursa na changamoto mbalimbali zinazokabili uendeshaji wa biashara ya Benki yetu,"aliongeza.

Aliipongeza Bodi na Uongozi wa Benki ya CRDB kwa kuendelea kutoa elimu kuhusu masuala ya hisa kwa wanahisa na wananchi wote kwa ujumla. Hata hivyo, alitaka juhudi hizo ziongezwe kwani alisema uelewa kuhusu masuala ya hisa bado ni mdogo miongoni mwa watanzania wengi.



*Mwanahisa wa Benki ya CRDB Bw. Salim Mbonde akibadilishana mawazo na Mwakilishi kutoka International Finance Corporation( IFC) Bw. Roman Zyla wakati wa Mkutano Mkuu uliofanyika jijini Arusha tarehe 20 Mei, 2017.*

"Watanzania inabidi tuamke na tuwekeze kwa kununua hisa," alisema Mzee Mbonde ambaye alianza kwa kununua hisa 100 zaidi ya miaka kumi iliyopita na hadi sasa anamiliki hisa takribani 200,000. Mzee Mbonde ni miongoni mwa kundi la wanahisa wenye hisa chini ya asilimia 1, ambao ni asilimia 44.8 ya hisa zote za Benki ya CRDB.

Anasema anapata faida mbalimbali kwa kuwa mwanahisa wa CRDB, mojawapo ni kupata gawio kila mwaka. "Hivi sasa nakula faida baada ya kuwekeza,"anasema. Aliongeza kuwa uwekezaji wake katika hisa za CRDB ni akiba ambayo anaweza kuitumia kwa kuuza hisa zake ikibidi kufanya hivyo.

Gharama za kuhudhuria Mkutano Mkuu na Semina kila mwaka ni moja ya changamoto anazokabiliana nazo, ingawa anakiri kuwa ni muhimu kwa kila mwanahisa kujitahidi kuhudhuria ili kujifunza na kujua maendeleo ya benki yao.

# Malipo ya Gawio kwa Mwaka 2016

Miongoni mwa maazimio ya Mkutano Mkuu wa 22 uliofanyika tarehe 20 Mei 2017 ilikuwa ni kuidhinishwa kwa gawio la shilingi 10 kwa kila hisa kwa mwaka ulioishia Desemba 2016, ambapo jumla ya shilingi bilioni 26.1 zitalipwa. Jumla ya gawio imepungua kwa asilimia 41 kutoka shilingi bilioni 44.4 iliyolipwa mwaka 2015.

Malipo ya Gawio kuanzia Mwaka 2011 hadi 2016 (thamani katika shilingi)

| Kipengele | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Gawio kwa kila hisa | 9 | 12 | 14 | 15 | 17 | 10 |
| Jumla ya Malipo ya Gawio | Bilioni 19.5 | Bilioni 26.1 | Bilioni 30.4 | Bilioni 32.6 | Bilioni 44.4 | Bilioni 26.1 |
| Ongezeko kwa asilimia | | 33 | 17 | 7 | 36 | -41 |

Benki ya CRDB inapenda kuwafahamisha wanahisa wake kuwa malipo ya gawio kwa Mwaka 2016 kwa wanahisa wake yalianza kufanyika tarehe 2 Juni 2017 kwa wanahisa waliokuwemo kwenye daftari la wanahisa lilipofungwa tarehe 11 Mei 2017.

Kwa Wanahisa ambao hawajawasilisha namba zao za akaunti za benki, wanaombwa kufanya hivyo mara moja ili malipo yafanyike kupitia akaunti zao. Kwa wanahisa ambao watapokea taarifa ya gawio *(Dividend Notice)* kupitia anuani zao za Posta wanatakiwa kwenda katika matawi ya Benki ambako wataelekezwa kufungua Akaunti ili malipo yao yaingizwe kwenye akaunti hizo.

Benki ya CRDB pia inapenda kuwakumbusha wanahisa wote kuwa malipo ya gawio hayafanyiki kwa fedha taslimu na badala yake yanaingizwa moja kwa moja kwenye akaunti za benki.

Wanahisa wote wanahimizwa kufungua akaunti za benki na kuwasilisha taarifa za akaunti zao pamoja na namba za simu na anuani za barua pepe kwa Katibu wa Benki. Namba ya simu pamoja na anuani ya barua pepe vitatumika kumtaarifu mwanahisa pale malipo yatakapofanyika pamoja na mawasiliano mengine muhimu.

# Je wajua taratibu za kudai gawio?

Wanahisa wa Benki ya CRDB wanawajibika kufahamu vizuri taratibu za kufuata ili kupata huduma kwa ufanisi, urahisi, wepesi na haraka. Kufahamu taratibu huepusha kutoelewana na malalamiko yasio ya lazima yanayoweza kutokea kati ya Wanahisa na kampuni walikowekeza. Uelewa mzuri wa taratibu hufanikisha mahusiano rafiki na ya wazi kati ya Mwanahisa na Kampuni husika. Faida nyingine ya kufahamu taratibu ni kumwezesha Mwanahisa kupata faida kutokana na uwekezaji wake na kuleta matokeo chanya na yaliyotarajiwa kutoka taasisi inayotoa huduma.Benki ya CRDB hutoa huduma za aina mbalimbali kwa Wanahisa wake kama vile;

- Kupokea na kushughulikia madai ya malipo ya gawio
- Mirathi: Kuhamisha Hisa kutoka kwa marehemu kwenda kwa mrithi
- Mwanahisa kubadili Jina
- Mwanahisa kubadili anuani
- Upotevu wa Stakabadhi ya Umiliki wa Hisa – binafsi
- Upotevu wa Stakabadhi ya Umiliki wa Hisa – Vikundi na kampuni
- Kuunganisha stakabadhi za Hisa

Benki ya CRDB imepewa kibali na Soko la Hisa la Dar es Salaam kutoa huduma tajwa hapo juu kwa wanahisa wake tu. Kati ya huduma ambazo zimekuwa zikiibua malalamiko miongoni mwa Wanahisa mara kwa mara ni madai ya kutolipwa gawio kwa wakati au kama inavyostahili. Hata hivyo, imebainika kuwa malalamiko au madai hayo yanatokana na Wanahisa kutofahamu vizuri taratibu zinazotakiwa kufuatwa ili kupata huduma mbalimbali ikiwemo namna ya kudai gawio.

Kwa wanahisa ambao hawajachukua gawio kutokana na sababu mbalimbali wanapaswa kuandaa na kufanya yafuatayo:

- Kuandika barua ya maombi ya kulipwa gawio *(Application letter)*
- Kujaza fomu ya kuboresha kumbukumbu za Mwanahisa *(Shareholder Updation Form)*
- Ambatisha nakala ya Stakabadhi ya Umiliki wa Hisa *(copy of CDS Receipt)* au taarifa ya polisi endapo Stakabadhi ya Umiliki wa Hisa imepotea
- Ambatisha nakala ya kitambulisho kipya cha Taifa/Kura, Hati ya kusafiria *(Passport)* au leseni ya udereva

Vitu au taarifa hizo zinatakiwa kuwasilishwa katika ofisi ya Katibu kupitia anuani ifuatayo:

Katibu, Benki ya CRDB, Office Accommodation Scheme - Mtaa wa Azikiwe, Ghorofa ya 4
S. L. P. 268, Dar-es-Salaam.
Simu. na. 022 - 2117442 - 7, 2114237
Barua pepe John.Rugambo@crdbbank.com au shareholders@crdbbank.com
Au: Mkurugenzi/Meneja wa Tawi lolote la Benki ya CRDB

# Jinsi ya Kurithisha Hisa zako

Ni ukweli kuwa binadamu yeyote siku moja maisha yake yatakoma hapa duniani na angependa kuwepo na mpangilio wa namna mali zake zitakavyomilikiwa na mtu au watu anaowaacha hapa duniani. Ukijua wazi kuwa kifo hakikwepeki, basi huna budi kuweka utaratibu au maandalizi ya namna mali zako zitakavyorithiwa.

## Njia kuu za Kurithisha Hisa

Hisa ni miongoni mwa mali ambazo mwanahisa anaweza kurithisha kwa mtu au watu wengine kwa jinsi apendavyo. Ziko njia kuu mbili za kurithisha hisa kama ifuatavyo:

### (i) Wosia wa Kimaandishi

Wosia wa maandishi ni pale ambapo mwanahisa anatoa maelekezo ya urithi wa hisa zake kwa njia ya maandishi. Njia hii ni bora zaidi kwani huondoa utata wowote kuhusiana na matakwa ya marehemu kuhusu mali/hisa zake. Mtu ambaye anajua kusoma na kuandika, anaweza kuandika wosia wake ukishuhudiwa na watu wawili (mtu mmoja awe miongoni mwa ndugu zake na mwingine awe ni mtu yeyote anayeaminika). Mtu ambaye hajui kusoma na kuandika, ataweka dole gumba kwenye matakwa yake, na wosia huo ushuhudiwe na watu wanne (wawili kati ya hao wawe ndugu zake na wawili wawe watu wanaoaminika).

Vilevile, mtu anaweza kuandika wosia ukishuhudiwa na wakili na hivyohahitaji ndugu au marafiki kujua kilichomo kwenye wosia wake. Maelekezo yaliyoko ndani ya wosia hayatakiwi kuwa na utata, na badala yake mambo yote yawekwe bayana ili utekelezaji wake usikwame. Endapo kutatokea utata katika tafsiri ya yale mambo ambayo marehemu ameyaandika, mahakama itatoa tafsiri hiyo.

**(ii) Wosia wa Mdomo**

Wosia wa mdomo ni pale ambapo mwanahisa anatamka mrithi wa hisa zake na kutoa maelekezo kwa maneno ya mdomoni. Hii ni njia ambayo mara nyingi utekelezaji wake ni mgumu kwani inahitaji mashahidi waliosikia wosia huo na hivyo kuilazimu mahakama kupata ushahidi huo ili maamuzi yatolewe kuhusumgao au urithi wa mali/hisa za marehemu.

Endapo wosia utatamka wazi msimamizi wa mirathi ya mali ya marehemu msimamizi huyo atafanya majukumu yake na kutoa taarifa mahakamani jinsi alivyogawa mali/hisa za marehemu. Ikumbukwe kuwamwanahisa anaweza kumrithisha mtoto/watoto au mtu/watu hata kama wana matatizo ya akili. Kwa mtoto, hisa zitakuwa chini ya mwangalizi hadi mtoto atakapofikisha umri wa miaka 18. Kwa mtu mwenye tatizo la akili, hisa zitakuwa chini ya mwangalizi kwa manufaa ya mgonjwa husika.

Katika njia zote zilizotajwa hapo juu, utambulisho kamili wa mrithi wa hisa za marehemu utatolewa na mahakama. Kiujumla, kuandika wosia kunarahisisha mrithi kujulikana mapema na kupata amri ya mahakama. Kutokuandika wosia, husababisha mchakato wa kumpata mrithi kuwa mrefu ambao unahitaji vikao vya familia ambavyo mara nyingi hushindwa kufikia muafaka kuhusu usimamizi na hata umiliki wa hisa za marehemu.

Ofisi ya Katibu wa Benki inazo nakala rahisi za wosia kwa wanahisawatakaohitaji. Endapo mwanahisa alishatangulia mbele ya haki, ndugu au msimamizi wa mirathi anashauriwa kuwasiliana na maafisa wa Benki walioko matawini kwa maelekezo zaidi. Zifuatazo ni nyaraka zitakazohitajika:

- Barua ya maombi *(Applicant letter)*
- Cheti halisi cha Hisa *(Original CDS Receipt)*
- Barua ya mahakama ya uteuzi wa usimamizi wa mirathi *(Form No. IV)*
- *Amendment form*
- Nakala ya cheti cha kifo cha marehemu
- Muhtasari wa kikao cha ndugu *(Minutes)*
- Nakala ya kitambulisho cha taifa/kura/ hati ya kusafiria *(Passport)*
- Risiti ya Benki ya malipo ya shilingi 1000/-
- Nakala ya cheti cha kuzaliwa / cheti cha ndoa.

Baada ya taratibu zote kukamilika kwa msimamizi kuainisha mrithi/warithi ambao wataidhinishwa na mahakama, ndipo hati zote husika hupelekwa kwenye Soko la hisa la Dar es Salaam ambacho ni chombo pekee kinachoba dilisha jina kutoka jina la marehemu kwenda kwa msimamizi wa mirathi, kwenda kwa mrithi/warithi. Baada ya kukamilika kwa taratibu katika soko la hisa, mrithi atapatiwa cheti chake cha umiliki wa hisa. Wanahisa wanasha uriwa kuandika wosia kwani huepusha matatizo mengi ikiwemo mafarakano kwenye familia na uwezekano wa kupoteza hisa.

**"USIOGOPE KUANDIKA WOSIA KWANI UTAEPUSHA MAFARAKANO KWENYE FAMILIA YAKO"**

# MATUKIO KATIKA PICHA



Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa 22 wa Wanahisa wa Benki ya CRDB Bw. Abeid Mwasajone akitoa nasaha zake



Wanahisa wa Benki ya CRDB wakisali kabla ya kuanza kwa Mkutano Mkuu wa Mwaka katika ukumbi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (AICC) jijini Arusha tarehe 20 Mei, 2017




Mwezeshaji kutoka Benki ya CRDB Bw. Emmanuel Ng'ui akitoa mada wakati wa semina ya wanahisa iliyofanyika siku moja kabla ya Mkutano Mkuu



Wanahisa wakipiga kura kuchagua mjumbe mmoja wa Bodi kutoka kundi la wanahisa wenye hisa chini ya asilimia moja




Mjumbe mpya wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya CRDB Dkt. Neema Munisi akijinadi kwa wanahisa kabla ya kuchaguliwa katika nafasi hiyo




Mwakilishi wa Balozi wa Denmark Bw. Birger Fredriksson akifuatilia Mkutano Mkuu wa Wanahisa wa Benki ya CRDB

# Mama Faida na Baba Mtaji

